

# **Mnunuzi Na Awe Macho**

**na**

**J D Logan**

# **Mnunuzi Na Awe Macho**

**na**

**J D Logan**

**Novemba 5, 2011**

# Mnunuzi Na Awe Macho

Labda kichwa cha somo hili linaoneka geni kwa baadhi yenu. Awali ya yote, haya ni makala yaliyotolewa na Mungu, au sio? Alafu, unaandika kuhusu nini, J D?

Sawa, miaka michache iliopita niliandika makala kuhusu tafsiri tofauti tofauti ya Neno la Mungu ambapo nilionyesha ugumu tunaokumbana nao tunaposisitiza matumizi ya “Tafsiri Iliyoamriwa”, zaidi sana ikijulikana kama “Toleo la Mfalme Yakobo”. (King James Version).

Nilionyesha kwamba “Elizabethan” cha zamani ya Kiingereza ambapo kitabu hiki cha Mfalme Yakobo kimeandikwa, kwa vifungu vingine, ugumu wa kuelewa na, katika mifano mingine inaongoza vibaya. Hatalivyo, ninaamini kwamba maelezo ya kindani yapo katika mtiririko.

Siyo muhimu kweli kwamba ugumu huu ni matokeo ya tafsiri mbaya. Inavyojulikana sana, ni matokeo ya mabadiliko ya lugha ya Kiingereza. Lugha yetu ni mkusanyiko wa lugha nyingi na iko katika hali ya ubora. Maelezo yanayotumiwa kwa njia moja leo ni juma lijalo, mwezi, mwaka, ikitumika katika njia tofauti. Siyo tu kwamba INATUMIKA vibaya, lakini kwa nafasi ndogo ya muda INAKUA inakubaliwa kama “kawaida”.

Siyo mshangao, basi, baada ya miaka 400+ tunakumbana na magumu. Hii yote ni kweli, lakini hebu na tuweke hii pembeni kidogo kwa muda huu, na tuingie katika “hadithi nyingine”.

## Kaa Macho

Katika miaka yangu ya kuajiriwa kwa mafanikio, nilikuwa muuzaji, meneja, muuzaji nk. Kitu kimoja tuliyofundishwa, na ambacho nilijifunza kwa haraka, ilikuwa ni maana ya maelezo ya Kilatini, “Caveat emptor”, ambayo, kimsingi, humaanisha “Mnunuzi awe macho”.

Sasa nilikuwa nashughulika katika bidhaa nyingi na huduma. Ilikuwa muhimu kwamba mimi, kama mununuzi wa kubadilisha, niwe makini katika hukumu yangu.

Haraka nikajifunza kwamba ninapaswa kuwakataa wauzaji “uwanda” na nifanye maamuzi ya upole ya vitu vilivyopo mkononi, na kutenda sawasawa. Je haikuwa vyema, au kwa uchache haikuonekana vizuri? Kwa ufupi, (katika lugha ya useremala: “pima mara mbili, kata mata moja”) kuwa makini na kile unacho nunua!

Uchunguzi mmoja wa mwisho: kama mtu haoni umuhimu wa hili, kutembelea gari la kawaida lililotumika mara nyingi na kuongea na

muuzaji kwa uwazi itaelezea kile ninacho kimaniisha. “Mununuzi na awe macho!!”

Wakati mwingine katika shauku yetu ya kujifunza neno la Mungu, tunasisitiza katika matumizi zaidi ya kifungu cha “kisasa” cha Biblia (kwa ualisia ziko mamia). Tunasoma kitabu “kilichorudiwa” ambayo inasikika vyema, hivyo tunaweka Mfalme Yakobo pembeni ya meza na kuiacha ikusanye vumbi na kutumia toleo “bora”. Lakini kwanza, “mununuzi na awe macho!!” Kama tunataka kumuacha “rafiki wa zamani”, kwanza tunatafuta rafiki bora.

Watu wa Afrika wanamsema unaosema, “Mwanangu kama ukiuza haki yako ya msingi, hakikisha unappkea kitu chenye thamani mbadala.” AMEN!!

Inaokana kila mtu alikuwa na tafsiri yake aliyoipenda mwenye. Ni ipi iliyo “sahihi”? kiwango kilichorudiwa (Marekani au Kiingereza), Biblia iliyo hai, leo toleo la Kiingereza, mpya ya kimataifa, Biblia mpya ya Kiingereza, Biblia ya Yerusalemu (Katholiki)?

Yaliyo hapo juu ni mifano ya kazi ya kiuanafunzi kwa mfumo unaofahamika, kwa mitandao unaoweza kufanya kazi nzuri. Lakini cha msingi ni WANAWENZA?

Yanayojulikana miongoni mwa zingine ni kauli njema, kitabu cha Moffat, Wilson Diaglot, Filipino na Beck. Mtu “Mmoja huyu” tafsiri inavikolombwezo vingi ya kuvithibitisha. Je zinafaa kutumiwa? Salama? “Mununuzi na awe macho!!”

Kitu kimoja ambacho nimejifunza zaidi ya miaka ni kwamba hakuna tafsiri ILIYOKAMILIKA. Kwa ufafanuzi, ni kazi za wanadamu ambazo, kwa nia njema, zimeshindwa, ni nani awezaye, kufanya, na kukosa.

Muhimu zaidi sana (hasa katika swala la tafsiri ya “mtu moja”), kuna tabia ya kuandika upendeleo katika kitabu. “mnunuzi na awe macho!!”

## Baadhi si ya kawaida

### Mwanz 6:2

- [K.J.V) “...baadhi ya wana wa Mungu waliona mabinti wa wanadamu...”
- [Kiingereza Kipya] “...wana wa miungu waliona ... mabinti wa wanadamu...”

Ni kipi unaweza kuchagua ambayo ni sahihi? Mtihani mdogo wa halisi unaweza kufunua Kiyunani “Elohiym” kumaanisha “Mungu

mwenye uwezo”. Katika idadi ni umoja na haiwezi kuongelea cho chote (au ye yote) isipokuwa Mungu wa kwenye Biblia.

Kwa nini, sasa, hawa wanaotafsiri wanaweza kutoa kosa la namna hiyo? Kimsingi inaniweka mbali; hasa, wakati ambapo “Elohiym” uyo huyo anaongelewa juu ya “Mungu” isipokuwa mistari saba baadaye! (Mwanzo 6:9). Ni nini kilichofanya tofauti?

Kama mmoja angeweza kuwa wazi na tafsiri hii ya Mwanzo 6:2, angeweza kulazimishwa kusoma mustari wa 9 kama, “...alitembea na miungu... “Mimi kwa mmoja sinta kubali hili; “ni uongo”, kosa! Tena, “Mnunuzi na awe macho!!”

Katika swala hili K.J.V iko wazi sana kuliko “Biblia Mpya ya Kiingereza”.

## **Mdo. 20:7**

Kuelezea ninachokimaanisha, angalia kifungu hicho hapo juu. Hapa imewekwa katika maelezo ya wazi mapenzi ya Roho Mtakatifu katika kazi na ibada ya kanisa lisiloelewa la Kristo ambao ni mfano wetu.

- [K.J.V] “...*siku ya kwanza ya juma...*”
- [Filipo] “...*siku ya juma pili...*”
- [Mistari ya King cha Leo] “...*siku ya juma pili jioni...*”
- [Biblia ya Kiing. Kipya] “...*siku ya juma pili usiku...*”

Kwa tafsiri kumi na moja niliyo nayo mbele yangu, tatu zinaonyesha siku ambayo mitume walikutana “Siku ya juma pili”. Nane (na mengine mengi) inazungumzia “siku ya kwanza ya juma”

Zaidi, Thayer (Uk. 187) kinasema “siku ya kwanza ya juma”. Kitabu cha vine kinasema (Uk. 240) kuhusu Sabato, katika msembo ambao ‘wa’ kitu, bila kujumuisha Sabato, bali kuifuata.”

Angalia zaidi, kitabu cha Vine katika Marko 16:9, “Mapema...jioni. Jua lilipozama; (asubuhi) mapema, hii ilikuwa ni siku ya kwanza, Juma pili, siyo Jumamosi! Nimetumia hili ili kueleza kwamba siku ilikuwa ni siku ya kwanza ya juma na siku hiyo ilianza mapema, jioni.

Kwa nini, sasa, tafsiri tatu hizi usomeka kama kawaida? Iko zaidi ya uelewa wangu, lakini ni wazi kwamba mmoja anweza kuongozwa vibaya kama akiongozwa na kita cho chote kati ya hizi pekee. Tena, “Mnunuzi na awe macho!!”

## Ukumbusho

### Sehemu ya pili ya nusu ya Mdo. 20:7 inasoma kama ifuatavyo:

- [K.J.V] “...wanafunzi walipokutana katika kuumeza mkate...”
- [Beck] “...siku ya juma pili, tulipokutana kwa ajili ya chakula...”

Wengi, leo, wanaondoa umuhimu wa ushirika wa meza ya Bwana katika siku ya kwanza ya juma. Wengine wanashindana kwamba tukio hili lilikuwa ni la chakula kama chakula cha usiku. nk.pasipo na kiashirio yo yote. Hataivyo, Luka, mwandishi wa kitabu cha Matendo ya Mitume, anaonyesha kwamba hii ndiyo ilikuwa sababu ya kukutana pamoja.

Paulo alihubiria kusanyiko kuhusu swala hili (mahubiri marefu sana). Katika 1 Kor. 11:22, analiagiza kanisa la Korintho kwamba tuna nyumba za kulia na kunywea. Wanafunzi hawakuhitaji “kukutana” ili wanywe na kula!

Tunaambiwa (Mdo. 2:42) “...walidumu katika fundisho la Mitume, na katika ushirika, na katika kuumeza mkate na katika kusali.” Haya ni matendo ya ibada, sio wajibu wa kila siku. “Wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu wote” (Mdo. 2:47) inaonyesha kwamba vitu hivi vilionekana hadharani na “kuonwa na watu”; kwa ufupi, ibada ya jumla.

Vile vile, katika Mdo. 20:7. hiki hakikuwa chakula cha kawaida, ndiyo maana walikutanika pamoja. Ilikuwa ushirika wa meza ya Bwana!!

Kwa nini Beck alitafsiri kifungu hiki? Sina uelewa katika swala hili. Nafahamu inamwongoza mtu katika hitimisho mbaya. K.J.V. ni sahihi! Beck hayuko sahihi! “Mnunuzi na awe macho!!”

Nimeona haya (kosa) tafsiri mbaya kueleza neno. Tunapaswa kuwa makini tunapo jaribu kuwashawishi wengine watumie tafsiri sahihi, au kuacha ile sahihi. Kuna mengine nzuri ambayo inaweza kupatikana katika tafsiri nyingi, iwe ya kisasa au ya zamani. Pia kuna makosa ya kuepuka. Nini, basi, tunaweza kutazama matatizo haya?

## Linganisha, linganisha, linganisha

Ukilinganisha tafsiri nyingi katika mustari wo wote ni msaada nzuri sana kila mara. Msaada mzuri katika kujifunza kwangu ni Tafsiri ya Nane ya Agano Jipya na Tyndale House Publisher. Hii inaweza kununuliwa katika maduka ya vitabu vingi.

Pia, tafsiri nyingi nzuri kama lexicon zinapatikana ambazo husomeka. Kitabu cha Vine Expository Neno la Kamusi ya Biblia inaeleweka kirahisi, maneno yamepangwa katika mtiririko wa kamusi.

Konkodance ya Strong ni ya muhimu sana. Inajumuisha mambo mengi, ukijumuisha kamusi ya Kiyunani na Kiebrania iliyoandikwa kwa Kiingereza, na ikaunganishwa kwa mfumo wa nambari ambayo ni rahisi kusoma.

## **Acha**

Baadhi ya tafsiri za “kisasa” inamuonyesha mwanafunzi kutoeshimu neno la Mungu.

Ulinganifu wa tafsiri nyingi itafunua hali ya kuachwa kwa mistari mingi. Wakati mwingine, mwandishi ataweka maandishi ya chini madogo madogo hali ya kuachwa huku, ikieleza kwamba mustari huu au ule siyo ya kifungu hiki au kwamba ilikuwa ni nyongeza mwandishi fulani au mhariri.

Nadhani mtu atanieleza jinsi mtu anavyoangalia pekee yake miaka 2000 baada ya hapo anaweza kuchagua kwamba mustari huo mmoja ni sahihi na nyingine inakosa na inapaswa kuachwa. Inaonekana kwangu kwamba kuwa na urefu wa ukatili unakuwa hakimu wa Neno la Mungu. Omba ili uweze kutolewa katika ukatili huo! “Mnunuzi na awe macho!!”

## **Kompiuta**

Programu nyingi za Kompiuta zinapatikana. Ulinganifu wa tafsiri unapatikana na ni nzuri.

Kitu kimoja cha kukumbuka, hataivyo, ni kwamba “vitabu” vinauthibitisho katika kompiuta si zaidi ya mawazo ya mwandishi. Zinaweza zikawa na mambo mazuri, au kuonyesha sehemu nzuri. Tena, nasema, “Mnunuzi na awe macho!!”

## **Kwa ufupi**

Tunaweza kufupisha kwa kusema kwamba tutakuwa tumeshauriwa vyema kutumia kila silaha inayopatikana katika maandiko. Lakini, zitumie kwa tahadhari!! Kabla hatuja tupilia mbali kazi yo yote ya mwandishi kwa sababu ye yote, lazima tuwe makini kwamba kile tunachokikubali katika mbadala wake ni bora sana. “Mnunuzi na awe macho!!”

Kwa uelewa mzuri wa ukweli,  
J D Logan







